## JAMHURI YA MUUNGANI WA TANZANIA

## OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA


SHULE YA SEKONDARI NEGERO

S.L.P 70

KILINDI-TANGA


**TAREHE...........................**


SIMU :**0621082429/0782665810**


Kumb Na:..........................................

MWANAFUNZI:...................................................................

**SHULE YA SEKONDARI NEGERO**

YAH:**<u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA MWAKA WA MASOMO 2021/2022</u>**

Husika na barua na kichwa cha habari hapo juu.

Kwa barua hii nakujulisha kuwa umechaguliwa kuingia kidato cha kwanza mwaka **2021/2022** shule ya Sekondari Negero unatakiwa kufika Shuleni kuanza masomo tarehe **05/01/2021** ufike kabla ya saa kumi (10:00) jioni shule hii ipo mkoa wa Tanga katika Wilaya ya Kilindi umbali wa kilometa 175 kutoka Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi kupitia Handeni.

Wanafunzi wote wapime afya zao na ajaziwe fomu iliyoambatanishwa ikiwa na taarifa ya Daktari.

Mkuu wa shule, walimu na wafanyakazi wote wa shule hii wanakupongeza na wanatarajia uwe mwanfaunzi MTIIFU, NADHIFU ,MWAMINIFU na MSHIRIKI mzuri wa kazi zote za nje na ndani ya darasa.

Kwa mawasiliano piga simu namba 0621082429/0782665810

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NEGERO**

MKUU WA SHULE S.L.P 70 KILINDI NEGERO SEKONDARI SIGNATURE

......................................

**MWAITA OMARI**

**MKUU WA SHULE**

## 1.0MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1.1 SARE YA SHULE

**A) WAVULANA;**

i. Suruali mbili (2) Rangi ya blue bahari zenye marinda kila upande.
ii. Mkanda mweusi.
iii. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi.
iv. Sweta rangi ya kijivu
v. Soksi nyeupe
vi. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba

**B) WASICHANA**

i. Siketi mbili (2) Rangi ya blue bahari, zivuke magoti mshono rinda boksi.
ii. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi.
iii. Sweta rangi ya kijivu.
iv. Soksi nyeupe.
v. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba visiwe na visigino virefu.
vi. Kwa waislamu washone sketi ndefu zinazofika kwenye kungu mbili. (karibu na kisigino) rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule.

**NB:**

**NI VEMA KUSHONEA SHULENI ILI KUEPUKA KUSHONA RANGI TOFAUTI**

### 1.2 VIFAA VYA USAFI.

Fagio, Jembe, Kwanja, Panga na ndoo ndogo

**HUDUMA ZA HOSTEL**

Shule yetu inatoa huduma ya Hostel kwa wasichana ambao wanaotoka mbali.

**MAHITAJI YA HOSTEL KWA WASICHANA NI KAMA IFUATAVYO**

1. Mahindi 70 kg kwa mhula mmoja.
2. Maharage 30 kg kwa mhula mmoja.
3. Mchele 6 kg kwa mhula.
4. Shilingi 50,000= kwa ajili ya viungo na mpishi.
5. Gharama ya kiingilio hostel ni Tshs 10,000/= kwa mwaka.
6. Shuka mbili (2), blue bahari 1 na pinki 1.
7. Aje na sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
8. Shamba dress ambazo hupatika na shule

NB. Mzazi atakaye mpangishia mototo wake nje ya shule jukumu la kumuangalia ni juu yake. Tunashauri watoto wote wa kike wakae hostel.

**2.0.SHERIA ZA SHULE.**

2.1.Mwanafunzi anatakiwa azingatie mambo yafuatayo;-

i. Kuhudhuria vipindi nyote vya darasani.
ii. Kutunza mali za shule na zauma kwa ujumla.
iii. Kushiriki vizuri katika kazi.
iv. Kuwahi katika kila shughuli.
v. Kusalimia walimu na walezi.
vi. Kuhudhuria mikutano yote ya shule.
vii. Kutokwenda nje ya shule bila kibali cha mwalimu.
viii. Haruhusiwi kutumia lugha mbaya shuleni.
ix. Kuvaa sare ya shule muda wote na kuzingatia ratiba ya shule.
x. Kuitika na kukimbia anapoitwa.
xi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

**2.2.MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA.**

i. Wizi.
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ubakaji.
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
v. Uvutaji bangi.
vi. Tumbaku n.k.
vii. Kupiga au kupigana.
viii. Kudharau bendera ya taifa na alama zingine za taifa mf .Wimbo wa Taifa
ix. Kuoa
x. Kusababisha mimba
xi. Kugoma au kuchochea mgomo
xii. Kakataa adhabu kwa makusudi
xiii. Kuwa na simu ya mkononi
xiv. Kuja na heater/kuwa na heater

**KARIBU SANA SHULE YA SIKONDARI NEGERO**

MKUU WA SHULE S. L. P 70 KILINDI ... NEGERO SEKONDARI

.....................................

**MWAITA OMARI**

**MKUU WA SHULE**

**UTHIBITISHO WA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI NEGERO**

**SEHEMU A (Ijazwenamwanafunzi**

Mimi (Jinakamili) ..........................................................................

Tarehe ya Kuzaliwa :.......................................................................

Dini ..................................................................................................

Kijiji ............................ Wilaya: ...................... Mkoa: ...........................

Nakubali nafasi niliopewa ya kuingia kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Negero Nathibitisha kuwa Ninatii na kufuata sheria zote za Shule kama zilivyo ainishwa. Najua nakuamini kuwa migomo na vurugu si njia sahihi ya kutatua matatizo katika jamii hivyo naahidi kutoshiliki katika Migomo wala vurugu zozote bali nitakuwa mstari wa mbele kutoa taarifa kwa Uongozi wa Shule ili matatizo yatafutiwe ufumbuzi pindi yanapotokea.

Saini: ................................................
Tarehe:.....................................

**SEHEMU B (IjazwenaMzazi/Mlezi)**

Mimi (JiniKamili) ................................................Namba ya simu ..........................

Kijiji: .................................. Wilaya: ................................ Mkoa: ..........................

Nafurahi kupokea nafasi aliyoipata mtoto wangu Nitatekereza na kutimiza mahitaji yote ya mtoto wangu wakati wote kusaidiana na shule kumlea mtoto huyo kinidhamu na kimaadili.

SainiyaMzazi:................................................Tarehe: ......................................

Jina la Mtendaji wa kijiji: .................................................................................

Saini: ............................Tarehe:..............................Muhuri:...............................

**Jina la Mtendaji Kata:...........................................................................**

Saini:...............................Tarehe:.............................Muhuri.................................

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**KILINDI DISTRICT COUNCIL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

NEGERO SEKONDARY SCHOOL,

**P.O.BOX 70**

**KILINDI**

**DATE:.................................**

**MEDICAL OFFICER, GOVERNMRNT HOSPITAL**

**..................................................................................**

NAME OF STUDENT:**..................................................................**

Please examine the above named student to ascertain his finess for admission to pursue studies ..........................................

Headmaster Medical Certificate

(To be compreted by a Medical Officer)

I have examined the above named with regard to:-

Eyes:..........................................................................

Ears:..........................................................................

Chest:..........................................................................

Spleen:.......................................................................

Abdomen:....................................................................

Urine:.........................................................................

Stool:..........................................................................

Hemogrobin (Hb)..........................................................

I consider that: ...........................................................................

1. He is of good health, free from infectiousdiseases, worms, bilharzias anddd fit to Pursue studies.
2. He is now fit to retun to school after having been treated for ....................

...............................   ..........................

Name and Designation   Signature

Official Stamp:..........................   Date ..........................